

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



Karansi Secondary School
P. O. Box 235, Sanya Juu,
Email: karansisecondary@yahoo.com

KUMB.NA.KSS/J/FORM/I/2021/.....

JINA LA MWANAFUNZI

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KARANSI
WILAYA YA SIHA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2020**

1.0. UTANGULIZI.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika Shule ya **Sekondari Karansi** Mwaka 2020. Shule ipo umbali wa Km mbili (2) kutoka **Karansi Center**

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** saa 2:00 asubuhi

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1. SARE ZA SHULE.

- a) Wavulana suruali mbili (2) za kitambaa cha rangi ya **Dam ya mzee** zenye rinda mbili mbele, upana wa chini usiwe pungufu ya inchi 16 na Soksi pea 3 rangi **nyeupe**
- b) Wasichana watashona sketi mbili (2) za kitambaa cha rangi ya **Dam ya mzee**, ndefu za rinda box ambazo zitatakiwa kugusa vifundo vya visigino na sweta rangi ya kijani
- c) Kwa wote, Shati nyeupe za mikono mifupi mbili, socks pea 3 **nyeupe** kwa wasichanana na **kaki** kwa wavulana, viatu **vyeusi** vya Ngozi visivyo na visigino virefu, pia ni lazima viwe vya kufunga Kamba.
- d) Wale wanaovaa hijabu wavae sketi ndefu, shati na hijabu nyeupe.
- e) Sare za michezo kwa shirt za rangi ya **dark rk blue** na raba.

WA NA FOMU HII

2.2. MAHITAJI YA DARASANI.

Madaftari counter books 2 quire 09, mkebe wa hisabati, kalamu za kutosha, penseli, rula na vifutio. na begi la kubebea madaftari

2.3. VIFAA VYA USAFI

Wanafunzi wote waje na ndoo ya plastic mpya 1, jembe lenye pini jipya 1 na ufagio wa chelewa 01

2.4. HUDUMA YA CHAKULA.

Mzazi/Mlezi atahakikisha kuwa mtoto wake anapata huduma ya chakula shuleni. **Kamati ya chakula ya Wazazi** imeweka utaratibu mzuri kuhakikisha kuwa wazazi wanachangia chakula na Wanafunzi wanapata chakula cha mchana shuleni

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAISI – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni;

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- viii. Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Wizi.
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuwa Mjamzito/ Kupata mimba.
9. Kuoja au Kuolewa.
10. Kutoa Mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi. 13. Kuwa na simu ya mkononi.


4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheri, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

NB: - Kwamzaziyeyote ambaye atampeleka mtoto wake shule yabinafsi alete uhibitisho kamili wa usajili wa mwanafunzi wa shule husika.

KARIBU SANA



SAID A. NGAGAMA.
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
KARANSI SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 235 SANYA JUU